

JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

BUNGE LA TANZANIA



ORODHA YA SHUGHULI ZA LEO

MKUTANO WA KUMI NA SITA

KIKAO CHA NANE

12 SEPTEMBER, 2019



ORODHA YA SHUGHULI ZA LEO

MKUTANO WA KUMI NA SITA

KIKAO CHA NANE – TAREHE 12 SEPTEMBER, 2019

I. DUA:

II. HATI ZA KUWASILISHA MEZANI:

WAZIRI WA UJENZI, UCHUKUZI NA MAWASILIANO:

Taarifa ya Mwaka na Hesabu zilizokaguliwa za Mfuko wa Barabara kwa Mwaka 2015/2016 (The Annual Report and Audited Report of Roads Fund Board for the year 2015/2016).

MWANASHERIA MKUU WA SERIKALI:

Maelezo ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali kuhusu Muswada wa Sheria ya Marekebisho ya Sheria Mbalimbali (Na. 6) wa Mwaka 2019 [*The Written Laws (Miscellaneous Amendments) (No. 6), Bill, 2019*].

MWENYEKITI WA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA SHERIA NDOGO:

Maoni ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Sheria Ndogo kuhusu Muswada wa Sheria ya Marekebisho ya Sheria Mbalimbali (Na. 6) wa Mwaka 2019 [*The Written Laws (Miscellaneous Amendments) (No. 6), Bill, 2019*].

MSEMAJI MKUU WA KAMBI RASMI YA UPINZANI BUNGENI KUHUSU WIZARA YA KATIBA NA SHERIA:

Maoni ya Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni kuhusu Muswada wa Sheria ya Marekebisho ya Sheria Mbalimbali (Na. 6) wa Mwaka 2019 [*The Written Laws (Miscellaneous Amendments) (No. 6), Bill, 2019*].

III. MASWALI KWA WAZIRI MKUU:

IV. MASWALI YA KAWAIDA:

OFISI YA WAZIRI MKUU:

99. MHESHIMIWA MUHAMMED AMOUR MUHAMMED (BUMBWINI):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri Mkuu:- Idadi ya Watu wenye Ulemavu inakaribia asilimia 10 ya Watanzania, na idadi hiyo inatarajiwa kuongezeka kwa sababu mbalimbali:-

Je, Serikali imejipanga vipi katika kuzisaidia na kuwezesha Taasisi zinazoshughulikia Watu wenye Ulemavu nchini.

OFISI YA RAIS (TAMISEMI):

100. MHESHIMIWA JOEL MWAKA MAKANYAGA (CHILONWA):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais (TAMISEMI):-

Je, Serikali ina mpango gani wa kuitengeneza barabara inayounganisha Kijiji cha Bwawani kilichopo Kata ya Manchali na Kijiji cha Ikowa kilichopo Kata ya Ikowa ili iweze kupitika katika kipindi chote cha mwaka.

WIZARA YA UJENZI, UCHUKUZI NA MAWASILIANO:

101. MHESHIMIWA ALLAN JOSEPH KIULA (IRAMBA MASHARIKI):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano:- Sera ya Serikali ya Awamu ya Tano ni kuunganisha Mikoa kwa barabara za lami:-

Je, ni lini Serikali itajenga barabara ya lami inayounganisha Mikoa ya Simiyu na Singida kupitia daraja la Sibiti lililopo Wilaya ya Mkalama.

WIZARA YA MALIASILI NA UTALII:

102. MHESHIMIWA OSCAR RWEGASIRA MUKASA (BIHARAMULO MAGHARIBI):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Maliasili na Utalii:- Mwanzoni mwa mwaka 2016 Wananchi wa Kijiji cha Kabukome Kata ya Nyarubungo Wilaya ya Biharamulo walivamiwa na Tembo na kupoteza asilimia kubwa ya mazao yao:-

Je, ni lini Wananchi hao watapata fidia ya mazao yao.

WIZARA YA FEDHA NA MIPANGO:

103. MHESHIMIWA JAKU HASHIM AYOUB (BLW):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Fedha na Mipango:-

- (a) Je, ni lini Benki ya FBME italipa Wateja amana zao zilizokuwepo kwenye Benki hiyo;
- (b) Je, Benki hiyo iko katika hali gani kwa sasa;
- (c) Je, Benki Kuu ya Tanzania ina dhamana gani katika kulinda mabenki.

WIZARA YA VIWANDA NA BIASHARA:

104. MHESHIMIWA HAWA ABDULRAHMAN GHASIA (MTWARA VIJIJINI):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Viwanda na Biashara:-

Je, ni nini mpango wa Serikali katika kuendeleza eneo la EPZA Mkoani Mtwara.

WIZARA YA KILIMO:

105. MHESHIMIWA DANIEL NICODEMUS NSANZUGWANKO (KASULU MJINI):

- Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Kilimo:- Nchi yetu kwa muda sasa imekumbwa na uhaba mkubwa wa mbegu hasa za Mahindi na Maharage ambayo ni mazao ya chakula; kwa taarifa zilizopo Wizara ya Kilimo (2018) nchi yetu inazalisha mbegu hizo kwa asilimia zisizozidi 35:-
 - (a) Je, kuna mkakati gani wa kutatua tatizo hilo ili angalau nchi itosheleze kwa asilimia 70;
 - (b) Je, ni kwa nini shamba la mbegu la Bugaga lililopo Wilaya ya Kasulu lisiwe kitovu cha kuzalisha mbegu za Mahindi na Maharage;
 - (c) Je, ni kwa nini Serikali haiwekezi katika uzalishaji wa mbegu hizo.

106. MHESHIMIWA ZAYNAB MATITU VULU (VITI MAALUM):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Kilimo:- Zao la Nazi lina faida nyingi sana kuanzia mti, matawi na Nazi yenyewe:-

(a) Je, ni lini Serikali itatafuta soko la kudumu la zao hilo;

(b) Je, Serikali ina mpango wa kuhamasisha kilimo cha zao hilo kama ilivyokuwa zamani.

WIZARA YA MAJI:

107. MHESHIMIWA INNOCENT SEBBA BILAKWATE (KYERWA):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Maji:- Usanifu na upembuzi wa kina wa Mradi wa maji wa Vijiji 57 Wilayani Kyerwa umekamilika muda mrefu:-


Je, ni lini utekelezaji wa mradi huo utaanza ili Wananchi wa Kyerwa waweze kupata maji safi na salama.

WIZARA YA HABARI, UTAMADUNI, SANAA NA MICHEZO:

108. MHESHIMIWA DEVOTHA MATHEW MINJA (VITI MAALUM):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Habari, Utamaduni, Sanaa na Michezo:- Timu ya soka ya Taifa ya Wanawake (Twiga Stars) imefanya vizuri na kulitea Taifa heshima miaka iliyopita na hivi karibuni:-

Je, ni upi mkakati wa Serikali wa kuhamasisha soka kwa Wanawake katika ngazi za Wilaya na Mikoa kuwa na timu za soka za Wanawake kama ilivyo kwa Wanaume.



V. MISWADA YA SHERIA YA SERIKALI:



***(Kusomwa Mara ya Pili, Kamati ya Bunge Zima na
Kusomwa Mara ya Tatu)***

Muswada wa Sheria ya Marekebisho ya Sheria Mbalimbali (Na. 6) wa Mwaka 2019 [*The Written Laws (Miscellaneous Amendments) (No. 6), Bill, 2019*].

**DODOMA
12 SEPTEMBER, 2019**

**S. KAGAIGAI
KATIBU WA BUNGE**